**BUNGE LA 13 | KIPINDI CHA 4**
**SENETI**

# KWA KANUNI YA MSWADA WA KATIBA YA KENYA (MAREKEBISHO), 2025 (MISWADA YA SENETI NAMBARI 13 YA 2025)

## FOMU YA MAONI YA UMMA

(*Kwa mujibu wa Ibara za 118 na 256 za Katiba na kanuni ya kudumu 145(5) ya Kanuni za Kudumu za Seneti).*

---

**Sehemu ya A — Taarifa ya Kibinafsi**

**1.** Jina kamili: ______________________________

**2.** Jinsia: ______________________________

**3.** Umri: ______________________________

**4.** Kaunti: ______________________________

**5.** Nambari ya Utambulisho (*Kitambulisho cha Taifa/Pasipoti/Leseni ya Udereva ya Kenya):* ____________

**Sehemu ya B — Maoni kuhusu Marekebisho Yanayopendekezwa katika Katiba**

Je, maoni yako ni yapi kuhusu Marekebisho yanayopendekezwa? (Weka alama sahihi na utoe sababu)

**1. Rekebisho linalopendekezwa kwa Ibara ya 94 ya Katiba ili kubainisha kwamba utungaji wa sheria, uwakilishi na uangalizi ni jukumu la Bunge la Taifa na Seneti.**

| | |
|---|---|
| ☐ Ninaunga mkono | *Sababu:* |
| ☐ Siungi mkono | *Sababu:* |
| ☐ Mengine | *Eleza:* |

**2. Rekebisho linalopendekezwa kwa Ibara ya 95 ili kubainisha kwamba uamuzi wa mgao wa mapato, uidhinishaji wa matumizi ya fedha, na uangalizi wa mapato ya taifa ni jukumu la Bunge la Taifa na Seneti.**

| | |
|---|---|
| ☐ Ninaunga mkono | *Sababu:* |
| ☐ Siungi mkono | *Sababu:* |
| ☐ Mengine | *Eleza:* |

**3. Rekebisho linalopendekezwa kwa Ibara ya 96 ili kuweka kisheria jukumu la uwakilishi wa Seneti kwa makundi maalum, kutoa nafasi kwa Seneti katika utungaji wa sheria, majadiliano na utatuzi wa masuala ya maslahi ya umma na kubainisha kwamba jukumu la uangalizi la Seneti linahusisha mapato ya taifa yanayogawanywa kwa kaunti pamoja na mapato yanayokusanywa na kaunti zenyewe.**

| | |
|---|---|
| ☐ Ninaunga mkono | *Sababu:* |
| ☐ Siungi mkono | *Sababu:* |
| ☐ Mengine | *Eleza:* |

4. **Rekebisho linalopendekezwa kwa Ibara ya 108 ili kutoa utaratibu wa ukuu na uongozi katika Seneti. Kwa sasa, Katiba inatoa tu utaratibu wa vyeo na uongozi katika Bunge la Taifa.**

| | |
|---|---|
| ☐ Ninaunga mkono | *Sababu:* |
| ☐ Siungi mkono | *Sababu:* |
| ☐ Mengine | *Eleza:* |

5. **Rekebisho linalopendekezwa kwa Ibara ya 109 ili kuweka utaratibu wa kuanzisha Mswada wowote katika Bunge la Taifa au Seneti, isipokuwa Mswada wa kukusanya mapato ya kitaifa ambao unaweza kuanza tu katika Bunge la Taifa. Kwa sasa, Seneti inaweza kuanzisha na kushughulikia Miswada inayohusu serikali za kaunti pekee.**

| | |
|---|---|
| ☐ Ninaunga mkono | *Sababu:* |
| ☐ Siungi mkono | *Sababu:* |
| ☐ Mengine | *Eleza:* |

6. **Kufutiliwa mbali kwa Ibara ya 110 ya Katiba. Kwa sasa, Ibara ya 110 ya Katiba inafafanua "mswada unaohusu serikali za kaunti ni nini", jambo ambalo limekuwa likieleweka kwa njia nyingi tofauti.**

| | |
|---|---|
| ☐ Ninaunga mkono | *Sababu:* |
| ☐ Siungi mkono | *Sababu:* |
| ☐ Mengine | *Eleza:* |

7. **Rekebisho linalopendekezwa kwa Ibara ya 111 ili kubainisha kwamba Miswada ya ugavi (Mswada wa Ugavi wa Mapato kwa Kaunti au Mswada wa Ugavi wa Ziada wa Mapato kwa Serikali za Kaunti) inaweza kuanzishwa katika Seneti na miswada ya kuidhinisha matumizi ya fedha (Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha au Mswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Ziada ya Fedha) inaweza kuanzishwa na Bunge la Taifa. Kwa sasa, Ibara ya 111 inaweka utaratibu wa kushughulikia Miswada Maalum inayohusu serikali za kaunti.**

| | |
|---|---|
| ☐ Ninaunga mkono | *Sababu:* |
| ☐ Siungi mkono | *Sababu:* |
| ☐ Mengine | *Eleza:* |

8. **Rekebisho linalopendekezwa kwa Ibara ya 113 ili kuoanisha mchakato wa usuluhishi na mfumo mpya unaopendekezwa chini ya Ibara ya 109 na kuondoa Miswada ya Ugavi na Matumizi ya Fedha kutoka katika mchakato wa usuluhishi.**

| | |
|---|---|
| ☐ Ninaunga mkono | *Sababu:* |
| ☐ Siungi mkono | *Sababu:* |
| ☐ Mengine | *Eleza:* |

9. **Rekebisho linalopendekezwa kwa Ibara ya 114 ambayo inafafanua "Miswada ya Fedha." Kwa sasa, ufafanuzi huo umekuwa ukieleweka kwa njia tofauti.**

| | |
|---|---|
| ☐ Ninaunga mkono | *Sababu:* |
| ☐ Siungi mkono | *Sababu:* |
| ☐ Mengine | *Eleza:* |

**10. Rekebisho linalopendekezwa kwa Ibara ya 115 ili kuoana na rekebisho linalopendekezwa kwa Ibara ya 109 na kuhakikisha uthabiti.**

| | |
|---|---|
| ☐ Ninaunga mkono | *Sababu:* |
| ☐ Siungi mkono | *Sababu:* |
| ☐ Mengine | *Eleza:* |

**11. Rekebisho linalopendekezwa kwa Ibara ya 116 ili kutoa ufafanuzi ulio wazi kuhusu kuanza kutumika kwa sheria pale ambapo Rais hakutoa kibali kwa Mswada wala kuurejesha kwa Bunge.**

| | |
|---|---|
| ☐ Ninaunga mkono | *Sababu:* |
| ☐ Siungi mkono | *Sababu:* |
| ☐ Mengine | *Eleza:* |

**12. Rekebisho linalopendekezwa kwa Ibara mbalimbali ili kugawa jukumu la kuidhinisha uteuzi na kuondolewa mamlakani kwa Maafisa mbalimbali wa serikali ambao ni Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma, Mwenyekiti wa Tume ya Ugavi wa Mapato, Mdhibiti wa Bajeti, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, pamoja na Wenyekiti na makamishna wa tume za kikatiba kwa Bunge la Taifa na Seneti. Kwa sasa, idadi kubwa ya uidhinishaji wa maafisa wa serikali hufanywa na Bunge la Taifa.**

| | |
|---|---|
| ☐ Ninaunga mkono | *Sababu:* |
| ☐ Siungi mkono | *Sababu:* |
| ☐ Mengine | *Eleza:* |

**13. Rekebisho linalopendekezwa ili kutunga Ibara mpya ya 199A ili kuunda Hazina ya Bunge la Kaunti kwa kila bunge la kaunti.**

| | |
|---|---|
| ☐ Ninaunga mkono | *Sababu:* |
| ☐ Siungi mkono | *Sababu:* |
| ☐ Mengine | *Eleza:* |

**14. Rekebisho linalopendekezwa kwa Ibara ya 221 ili kuweka sawa mchakato wa bajeti kwa kuweka utaratibu wa kushughulikia na kuidhinisha makadirio ya bajeti katika Bunge la Taifa na Seneti. Kwa sasa, jukumu hili ni la Bunge la Taifa.**

| | |
|---|---|
| ☐ Ninaunga mkono | *Sababu:* |
| ☐ Siungi mkono | *Sababu:* |
| ☐ Mengine | *Eleza:* |

**15. Rekebisho linalopendekezwa kwa Ibara ya 222 ili kutoa utaratibu kwamba iwapo kupitishwa kwa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Fedha kutachelewa, utowaji wa fedha kutoka Hazina Kuu utaidhinishwa na Bunge la Taifa na Seneti. Kwa sasa, idhini hii inahitajika tu kutoka kwa Bunge la Taifa.**

| | |
|---|---|
| ☐ Ninaunga mkono | *Sababu:* |
| ☐ Siungi mkono | *Sababu:* |
| ☐ Mengine | *Eleza:* |

16. **Rekebisho linalopendekezwa kwa Ibara ya 223 inayoeleza kwamba idhini ya Bunge la Taifa na Seneti itahitajika pale ambapo fedha zinatumika kwa malengo ambayo hayakuidhinishwa. Kwa sasa, idhini hii inahitajika tu kutoka kwa Bunge la Taifa.**

| | |
|---|---|
| ☐ Ninaunga mkono | *Sababu:* |
| ☐ Siungi mkono | *Sababu:* |
| ☐ Mengine | *Eleza:* |

17. **Rekebisho linalopendekezwa kwa Ibara ya 224 ili kubainisha kwamba msingi wa maandalizi ya bajeti na serikali za kaunti ni Mswada wa Ugavi wa Mapato ya Kaunti na sio Mswada wa Kugawa Mapato, na kuanzisha mfumo unaoruhusu Bunge kuidhinisha utoaji wa muda wa fedha kutoka kwa Hazina Kuu kusaidia kaunti endapo kupitishwa kwa Mswada wa Kugawa au Mswada wa Ugavi wa Mapato ya Kaunti kutachelewa.**

| | |
|---|---|
| ☐ Ninaunga mkono | *Sababu:* |
| ☐ Siungi mkono | *Sababu:* |
| ☐ Mengine | *Eleza:* |

18. **Rekebisho linalopendekezwa kwa Ibara ya 250 ili kutoa ufafanuzi kwamba uidhinishaji wa uteuzi wa kamishna wa tume ya kikatiba au anayeshikilia wadhifa wa ofisi huru utashughulikiwa na Bunge la Taifa na Seneti. Kwa sasa, jukumu hili limepewa Bunge la Taifa.**

| | |
|---|---|
| ☐ Ninaunga mkono | *Sababu:* |
| ☐ Siungi mkono | *Sababu:* |
| ☐ Mengine | *Eleza:* |

19. **Rekebisho linalopendekezwa kwa Ibara ya 251 ili kutoa ufafanuzi kwamba kuondolewa mamkalani kwa kamishna wa tume ya kikatiba au anayeshikilia wadhifa wa ofisi huru kutashughulikiwa na Bunge la Taifa na Seneti. Kwa sasa, jukumu hili limepewa Bunge la Taifa.**

| | |
|---|---|
| ☐ Ninaunga mkono | *Sababu:* |
| ☐ Siungi mkono | *Sababu:* |
| ☐ Mengine | *Eleza:* |

20. **Maoni mengine yoyote kuhusu Mswada.**

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------------

**IMETIWA SAINI____________________TAREHE: ______________________________, 2025**

***Zingatia:***

*Fomu zilizojazwa zinaweza kutumwa kwa Katibu wa Seneti, S.L.P 41842-00100, Nairobi, kuwasilishwa moja kwa moja kwa Ofisi ya Katibu wa Seneti, Majengo ya Bunge, Nairobi au kutumwa kwa baruapepe kupitia maoni@parliament.go.ke na nakala kwa senatejlahrc@parliament.go.ke*

***Shukrani**: Seneti inathamini ushiriki wako katika mchakato huu.*

*"Kwa Ustawi wa Jamii na Utawala wa Haki kwa Wananchi"*